# HALMASHAURI YA WILAYA MASASI

*(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)*

Simu: 2510031,
**Fax: 2510045.**
E-mail: **ded.masasi@gmail.com**
**ded@masasi.go.tz**

S.L.P. 60,
**Masasi,**
Mtwara**,**

Tarehe: 23/02/2021.

MHESHIMIWA MWENYEKITI,
BARAZA LA MADIWANI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 60
**MASASI.**

**YAH: KUWASILISHA RASIMU YA MPANGO NA BAJETI YA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.**

Mhe; Mwenyekiti,

Naomba kuwasilisha rasimu ya Mpango na Bajeti ya Halmashauri kwa kipindi cha 2021/2022 umeandaliwa kwa kufuata Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka 5 Awamu ya II (FYDP II 2016/17 – 2020/21) Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi – CCM (2020-2025), Hotuba ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kuzindua Bunge la 12 na maelekezo mbalimbali ya Serikali, kitaifa, Wizara Mama TAMISEMI, Kimkoa na Kiwilaya yote kwa pamoja ikiwa na lengo la kuwatumikia wananchi na kuwaletea maendeleo endelevu.

Mhe; Mwenyekiti, Bajeti ya mwaka 2021/2022 imejikita zaidi katika kutekeleza mambo yafuatayo:-

1. Kuzingatia matumizi ya mfumo mpya wa ‘‘Web Based PlanRep’’ Unaotumiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa- MSM katika maandalizi ya Mipango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 badala ya mfumo wa zamani wa PlanRep ya kawaida

2. Kutenga bajeti kwa ajili ya kutekeleza masuala mtambuka kama vile jinsia, UKIMWI na virusi vya UKIMWI, watu wenye ulemavu, masuala ya lishe, ulinzi wa Mtoto, Vijana na Wazee pamoja na mazingira ya Mabadiliko ya Tabia Nchi

3. Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji na tathmini (M&E)

4. Kuweka kipaumbele kwa kutenga bajeti kwenye miradi ya maendeleo inayoendelea.

5. Kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kusaidia vikundi vya ujasiriamali vya wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu kwa mchanganuo ufuatao: - Wanawake 4%, Vijana 4% na 2% watu wenye ulemavu.

6. Kutenga asilimia 40 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kutumika katika miradi ya maendeleo na kipaumbele kitolewe kwenye kuwekeza ili kuimarisha vyanzo vikuu vya mapato.

   - ✓ Halmashauri kutenga 40% ya fedha zake za Mapato ya Ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na 60% Matumizi mengineyo. Sanjari na hilo imeelekezwa kuwa asilimia 40 ya fedha za Mapato zinazotokana na kilimo zikatumike kwenye Idara husika kwa machanganuo ufuatao (20% Kilimo, 15% Mifugo na 5% Uvuvi).

7. Kutenga bajeti kwa ajili ya kupanga matumizi bora ya ardhi katika maeneo ya Mijini na Vijijini na kushughulikia migogoro ya ardhi ili kuzuia migogoro ya wakulima na wafugaji.

8. Kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati na ujenzi ili kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na kijamii katika sekta zote mfano Afya, Elimu, Kilimo n.k kipaumbele kikiwa kwenye miradi ambayo haijakamilika iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

9. Kutenga bajeti asilimia 20 ya GPG kwa ajili ya uendeshaji wa Serikali za Vijiji.

10. Kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali, Vituo vya Afya na ukarabati wa Vituo vya kutolea huduma vilivyopo ili kuleta tija na kuboresha huduma za Afya.

11. Kutenga fedha kwa ajili ya kuimarisha masuala ya ulinzi na usalama na kuendesha vikao vya kisheria, pamoja na masuala ya kupambana na Rushwa.

12. Kutenga fedha kwa ajili ya masuala ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022

## A: MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI 2020/2021

Mhe; Mwenyekiti

Katika bajeti ya mwaka 2020/2021 Halmashauri ilikadiria kukusanya na kutumia jumla ya shilingi **34,639,132,000.00** kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Kati ya makisio hayo, shilingi **31,659,132,000.00** ilikuwa ni Ruzuku toka serikali Kuu, na shilingi **2,980,000,000.00** kutoka Mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mhe; Mwenyekiti, hadi Disemba 31, 2020, Halmashauri ilikuwa imepokea na kukusanya jumla ya shilingi **16,179,016,490.79** toka vyanzo vyake mbalimbali vya mapato, Fedha hizo ni sawa na asilimia **46.71** ya makisio.

**Jedwali Na.1 Mchanganuo wa mapato kwa kila fungu:-**

| Eneo | Makisio ya Mapato-H/W | Mapato Halisi hadi Disemba, 2020 | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| Mapato ya Ndani | 2,980,000,000.00 | 2,523,334,219.45 | 84.68 |
| **Jumla ya mapato ya ndani** | **2,980,000,000.00** | **2,523,334,219.45** | **84.68** |
| Ruzuku - Mishahara | 18,418,374,000.00 | 8,436,847,761.00 | 45.81 |
| Ruzuku–Matumizi mengineyo | 1,124,249,000.00 | 667,883,750.00 | 59.41 |
| Miradi ya Maendeleo | 12,116,509,000.00 | 1,489,102,763.00 | 12.29 |
| **Jumla ya vyanzo toka Serikali Kuu** | **31,659,132,000.00** | **9,104,731,511.00** | **28.76** |
| **Jumla Kuu Bajeti** | **34,639,132,000.00** | **13,117,168,493.45** | **37.87** |
| Fedha zilizopokelewa nje ya bajeti | 0.00 | 3,061,847,997.00 | 0.00 |
| **Jumla Kuu Bajeti + Nje ya Bajeti** | **34,639,132,000.00** | **16,179,016,490.79** | **46.71** |

**B: MATUMIZI:**

Mhe; Mwenyekiti,

Kwa upande wa Matumizi, mwaka 2020/2021 Halmashauri ilikadiria kutumia shilingi **34,639,132,000.00** Kati ya matumizi hayo **2,980,000.00** ni kutokana na vyanzo vya ndani, shilingi **31,659,132,000.00** ni kutokana na Ruzuku toka serikali Kuu kwa ajili ya Mishahara, Matumizi mengineyo na Miradi ya Maendeleo.

Mhe; Mwenyekiti hadi kufikia Disemba, 31 2020 Halmashauri imetumia jumla ya shilingi **15,064,913,287.45** sawa na asilimia **43.5** ya makisio.

**Jedwali Na.2 Mchanganuo wa Matumizi kwa kila fungu**

| Eneo | Makisio ya Matumizi- 2020/21 | Matumizi Hadi Disemba, 2020 | % Ya Matumizi Hadi Disemba |
|---|---|---|---|
| Mapato ya Ndani | 2,980,000,000.00 | 1,594,915,348.99 | 53.52 |
| **Jumla ya matumizi mapato ya ndani** | **2,980,000,000.00** | **1,594,915,348.99** | **53.52** |
| Ruzuku - Mishahara | 18,418,374,000.00 | 8,435,968,819.09 | 45.80 |
| Ruzuku–Matumizi mengineyo | 1,124,249,000.00 | 616,742,359.03 | 54.86 |
| Miradi ya Maendeleo | 12,116,509,000.00 | 1,410,438,763.00 | 11.64 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jumla ya vyanzo toka Serikali Kuu** | **31,659,132,000.00** | **10,463,149,941.12** | **43.67** |
| **Jumla Kuu** | **34,639,132,000.00** | **12,058,065,290.11** | **44.45** |
| Fedha zilizopokelewa nje ya bajeti | - | 3,006,847,997.34 | 0.00 |
| **Jumla Kuu** | **34,639,132,000.00** | **15,064,913,287.45** | **43.49** |

**C: MAPITIO YA MAPATO YA NDANI KUFIKIA DISEMBA, 2020.**

Mhe; Mwenyekiti, Jedwali Na.3 hapa chini linaonyesha mapato halisi ya fedha za ndani hadi kufikia Disemba 31, 2020.

| MAELEZO | MAKISIO YA MWAKA 2020/2021 | MAPATO JULAI-DISEMBA, 2020 | ASILIMIA % |
|---|---|---|---|
| **Ushuru wa Mazao:** | | | |
| Mahindi | 4,200,000.00 | 80,000.00 | 1.90 |
| Mpunga | 100,000.00 | 0.00 | 0.00 |
| Korosho | 1,356,480,000.00 | 1,258,843,113.00 | 92.80 |
| Ufuta | 300,000,000.00 | 163,763,668.00 | 54.59 |
| Mbaazi | 14,000,000.00 | 26,517,850.00 | 189.41 |
| Choroko | 8,000,000.00 | 0.00 | 0.00 |
| Karanga | 174,000.00 | 0.00 | 0.00 |
| Nyanya (Chidya) | 1,000,000.00 | 490,000.00 | 49.00 |
| Nyanya (Chiwata) | 1,000,000.00 | 905,500.00 | 90.55 |
| Nyanya/embe | | 7,354,502.00 | |
| **Mapato Kupitia Vyanzo Vingine** | | | |
| Nyumba za kulala wageni | 5,040,000.00 | 1,802,500.00 | 35.76 |
| Ushuru wa Huduma | 29,340,000.00 | 8,232,707.57 | 28.06 |
| Ushuru wa stendi | 66,600,000.00 | 19,290,800.00 | 28.97 |
| Leseni za Biashara | 32,845,000.00 | 12,210,000.00 | 37.17 |
| Leseni za vileo | 3,200,000.00 | 730,000.00 | 22.81 |
| Mazao ya Misitu | 1,000,000.00 | 573,700.00 | 57.37 |
| Mapato mengineyo | 14,805,000.00 | 28,868,589.00 | 194.99 |
| Ushuru wa Kokoto (CHIPITE) | 70,000,000.00 | 56,822,000.00 | 81.17 |
| Ushuru wa Kokoto (MKUNGU) | 12,000,000.00 | 10,837,500.00 | 90.31 |
| Ushuru wa Kokoto (BEIJING CONTRUCTION) | 20,000,000.00 | 10,000,000.00 | 50.00 |
| Ushuru wa Kokoto (MPODIPODI) | 45,000,000.00 | 41,963,500.00 | 93.25 |
| ushuru wa kokoto (MSANGA/MKANGAULA) | 3,000,000.00 | 4,862,000.00 | 162.07 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ada ya usajili vikundi | 800,000.00 | 560,000.00 | 70.00 |
| Ada ya Upimaji mashamba/ardhi | 10,400,000.00 | 283,000.00 | 2.72 |
| Ada ya Ukaguzi wa Nyama | 6,980,000.00 | 4,659,000.00 | 66.75 |
| Shamba la Halmashauri | 60,000,000.00 | 0.00 | 0.00 |
| Faini na Tozo | 5,000,000.00 | 1,910,000.00 | 38.20 |
| **Jumla ndogo Mapato ya Ndani** | **2,070,964,000.00** | **1,680,667,841.45** | **81.15** |
| **MAPATO LINDWA YA HALMASHAURI** | | | |
| Fedha za Elimu ya Kujitegemea (EK) | 86,278,000.00 | 85,017,650.00 | 98.54 |
| Mfuko wa Elimu | 517,750,000.00 | 654,729,728.00 | 126.46 |
| Papo kwa papo (User Fee) | 90,000,000.00 | 55,049,000.00 | 61.17 |
| Ada ya shule za Sekondari | 105,000,000.00 | 46,890,000.00 | 44.66 |
| Mfuko wa Dawa | 20,000,000.00 | 980,000.00 | 4.90 |
| iCHF | 60,000,000.00 | 0.00 | 0.00 |
| Bima (NHIF) | 30,008,000.00 | 0.00 | 0.00 |
| **Jumla ndogo Lindwa** | **909,036,000.00** | **842,666,378.00** | **92.70** |
| **Jumla ya Mapato ya Ndani** | **2,980,000,000.00** | **2,523,334,219.45** | **84.68** |

## D. MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021 – 2022 KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI.

Mhe; Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha **2021/2022** Halmashauri ya Wilaya ya Masasi inategemea kukusanya na kutumia jumla ya shilingi **44,397,290,000.00** kutoka vyanzo mbalimbali vya Halmashauri**.** Katika Fedha hizo shilingi **3,538,673,000.00** ni mapato ya Ndani ya Halmashauri na shilingi **40,858,617,000** ni Ruzuku toka Serikali kuu kwa ajili ya Mishahara, Matumizi mengineyo na Miradi ya Maendeleo.

Mhe; Mwenyekiti, kwa upande wa mapato ya ndani, Halmashauri imejipanga kukusanya jumla ya shilingi **3,538,673,000.00** kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato fedha ambazo zitatumika katika shughuli mbalimbali za serikali.

## E. MAPATO YA NDANI:

Kwa mwaka wa fedha **2021/2022** Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imepanga kukusanya jumla ya shilingi **3,538,673,000.00 (Sh. 2,285,766,000.00** mapato yasiyolindwa na shilingi **1,252,907,000.00** mapato lindwa**)** kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato, fedha hizo zitagawanywa katika sekta mbalimbali ili kutekeleza shughuli za kiutawala na miradi ya maendeleo.

Mhe, Mwenyekiti, Kiasi hiki kimeongezeka kwa asilimia **18.75** ukilinganisha na mwaka 2020/21 ambapo makisio yalikuwa shilingi **2,980,000,000.00**

**A: Jedwali Na.4: Kuonesha Mtiririko wa Mapato toka vyanzo Visivyolindwa**

<table>
<tr><th>KASMA</th><th>MAELEZO</th><th>MAKISIO 2021/2022</th></tr>
<tr><td>110815</td><td>

**Ushuru wa Mazao:**

Halmashauri inakisia kukusanya **Sh. 1,849,880,000.00** kutoka chanzo cha Ushuru wa mazao kwa mchanganuo ufuatao:

<table>
<tr><th>Zao</th><th>Tani Tegemewa (2021/22)</th><th>Bei kwa kilo</th><th>3% ya bei kwa kilo (Ushuru)</th><th>Kiasi tegemewa</th></tr>
<tr><td>Korosho</td><td>26,000</td><td>2,000</td><td>56.52</td><td>1,469,520,000</td></tr>
<tr><td>Ufuta</td><td>5,500</td><td>2,000</td><td>60.00</td><td>330,000,000</td></tr>
<tr><td>Mbaazi</td><td>500</td><td>800</td><td>40.00</td><td>20,000,000</td></tr>
<tr><td>Nyanya</td><td>12,000</td><td>**500</td><td>0.00</td><td>6,000,000</td></tr>
<tr><td>Embe</td><td>20,000</td><td>**500</td><td>0.00</td><td>10,000,000</td></tr>
<tr><td>Choroko</td><td>200</td><td>800</td><td>40.00</td><td>8,000,000</td></tr>
<tr><td>Mahindi</td><td>700</td><td>300</td><td>6.00</td><td>4,200,000</td></tr>
<tr><td>Mpunga</td><td>2.5</td><td>800</td><td>40</td><td>100,000</td></tr>
<tr><td>Karanga</td><td>2.0</td><td>1,000</td><td>30</td><td>60,000</td></tr>
<tr><td>Kochoko</td><td>2,000</td><td>1,000</td><td>***1,000</td><td>2,000,000</td></tr>
<tr><td>Jumla</td><td></td><td></td><td></td><td>1,849,880,000</td></tr>
</table>

** Ushuru wa Nyanya hutozwa kwa tenga<br>
** Ushuru wa Embe hutozwa kwa tenga<br>
*** Ushuru wa Kochoko hutozwa kwa gunia

</td><td>1,849,880,000.00</td></tr>
<tr><td>140384</td><td>

**Faini na adhabu:**

Halmashauri ya Wilaya ya Masasi inatarajia kukusanya **Sh. 1,692,000/=** kwa wastani wa **Sh. 141,000=** kwa mwezi.

</td><td>1,692,000.00</td></tr>
<tr><td>140376</td><td>Ushuru wa Mazao ya Misitu:</td><td></td></tr>
</table>

<table>
<tr><th>KASMA</th><th>MAELEZO</th><th>MAKISIO 2021/2022</th></tr>
<tr><td></td><td>Halmashauri inatarajia kukusanya jumla ya Sh. 1,000,000/= kutokana na maliasili zilizopo katika Halmashauri kama ifuatavyo:<br><br>Ushuru wa misitu<br><br>(ushuru wa 5%)<br><br>Mbao $m^3$ 200@5,000 sh. 1,000,000/=<br><br>Jumla sh. 1,000,000/=</td><td>1,000,000.00</td></tr>
<tr><td>110851</td><td>Ushuru wa Huduma (Service Levy):<br><br>Halmashauri inategemea kukusanya Sh. 34,240,000/= kutokana na huduma zinazotolewa na Wafanyabiashara (Viwanda) ndani ya Wilaya.<br><br>
<table>
<tr><th>Chanzo</th><th>Ushuru/mwezi</th><th>Miezi</th><th>Jumla</th></tr>
<tr><td>Ndanda spring</td><td>300,000</td><td>12</td><td>3,600,000</td></tr>
<tr><td>Ndanda Abbey</td><td>140,000</td><td>12</td><td>1,680,000</td></tr>
<tr><td>Ndanda Printing</td><td>80,000</td><td>12</td><td>960,000</td></tr>
<tr><td>Drumax</td><td>200,000</td><td>12</td><td>2,400,000</td></tr>
<tr><td>Mawasiliano ya simu</td><td>133,000</td><td>12</td><td>4,000,000</td></tr>
<tr><td>NMB Ndanda</td><td>120,000</td><td>12</td><td>1,440,000</td></tr>
<tr><td>Nanganga Petrol station</td><td>90,000</td><td>12</td><td>1,080,000</td></tr>
<tr><td>Ndanda Mission Petrol Station</td><td>80,000</td><td>12</td><td>960,000</td></tr>
<tr><td>Mkalapa Petrol Station</td><td>70,000</td><td>12</td><td>840,000</td></tr>
<tr><td>Ukod Oil International</td><td>50,000</td><td>12</td><td>600,000</td></tr>
<tr><td>JK Oil</td><td>50,000</td><td>12</td><td>600,000</td></tr>
<tr><td>LSS Petrol station</td><td>50,000</td><td>12</td><td>600,000</td></tr>
<tr><td>Dolphin Petrol Station(Lukuledi)</td><td>50,000</td><td>12</td><td>600,000</td></tr>
<tr><td>Wakandarasi</td><td>200,000</td><td>12</td><td>2,400,000</td></tr>
<tr><td>Wazabuni</td><td>150,000</td><td>12</td><td>1,800,000</td></tr>
<tr><td>Ndanda workshop</td><td>120,000</td><td>12</td><td>1,440,000</td></tr>
</table></td><td>34,240,000.00</td></tr>
</table>

<table>
<tr><th>KASMA</th><th>MAELEZO</th><th>MAKISIO 2021/2022</th></tr>
<tr><td></td><td>
<table>
<tr><td>Pepsi</td><td>100,000</td><td>12</td><td>1,200,000</td></tr>
<tr><td>Cocacola</td><td>110,000</td><td>12</td><td>1,320,000</td></tr>
<tr><td>TBL</td><td>160,000</td><td>12</td><td>1,920,000</td></tr>
<tr><td>SBL</td><td>150,000</td><td>12</td><td>1,800,000</td></tr>
<tr><td>Madini</td><td>250,000</td><td>12</td><td>3,000,000</td></tr>
<tr><td>JUMLA</td><td></td><td></td><td>34,240,000</td></tr>
</table>
</td><td></td></tr>
<tr><td>110852</td><td>Hoteli na Nyumba za Wageni:<br><br>Halmashauri inakisia kukusanya Sh. 10,800,000/= kutokana na nyumba 30 za kulala wageni pamoja na hoteli wastani wa Sh. 900,000/= kila mwezi x miezi 12</td><td>10,800,000.00</td></tr>
<tr><td>140370</td><td>Leseni za Vileo (Other Business Licence Fees):<br><br>Halmashauri inakisia kukusanya Sh. 2,160,000/= kutokana na<br><br>1. Leseni za pombe za kigeni, Halmashauri ina jumla ya grocery 24@ 90,000 Sh. 2,160,000</td><td>2,160,000.00</td></tr>
<tr><td>140353</td><td>Kokoto,Mawe na Mchanga (Madini ya Ujenzi)<br><br>Halmashauri inakadiriwa kukusanya kiasi cha Sh. 210,000,000/= kutoka mradi wa uuzaji wa kokoto, mawe na mchanga. Shilingi 17,500,000*12</td><td>210,000,000.00</td></tr>
</table>

<table>
<tr><th>KASMA</th><th>MAELEZO</th><th>MAKISIO 2021/2022</th></tr>
<tr><td>140371</td><td>Leseni za Biashara<br>Kiasi cha sh. 36,715,000 zinakadiriwa kukusanywa kutokana na utoaji wa leseni za biashara kama ifuatavyo:-
<table>
<tr><td>AMCOS Matawi Makuu</td><td>50 @ 40,000/=</td><td>2,000,000</td></tr>
<tr><td>Maduka ya vifaa vya ujenzi</td><td>75@ 65,000/=</td><td>4,875,000</td></tr>
<tr><td>Maduka ya Jumla</td><td>29 @ 100,000/=</td><td>2,900,000</td></tr>
<tr><td>Maduka ya rejareja</td><td>250 @ 50,000/=</td><td>12,500,000</td></tr>
<tr><td>Viwanda vya Maji</td><td>2 @ 300,000/=</td><td>600,000</td></tr>
<tr><td>Maduka ya dawa baridi</td><td>70 @ 100,000/=</td><td>7,000,000</td></tr>
<tr><td>Maduka ya pembejeo za kilimo/mifugo</td><td>14@ 60,000/=</td><td>840,000</td></tr>
<tr><td>Bucha za nyama/samaki</td><td>25 @ 30,000/=</td><td>750,000</td></tr>
<tr><td>Nyumba za kulala wageni</td><td>30 @ 80,000/=</td><td>2,400,000</td></tr>
<tr><td>Mashine za kusaga nafaka</td><td>120 @ 20,000/=</td><td>2,400,000</td></tr>
<tr><td>Huduma za fedha kwenye simu</td><td>30@ 15,000/=</td><td>450,000</td></tr>
<tr><td>JUMLA</td><td></td><td>36,715,000</td></tr>
</table></td><td>36,715,000.00</td></tr>
<tr><td>140368</td><td>Mapato Mengineyo<br>Halmashauri inatarajia kukusanya kiasi cha shs. 14,805,000.00 /= kutokana na ukusanyaji wa vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo havijakisiwa.</td><td>14,805,000.00</td></tr>
<tr><td>140293</td><td>Ada ya Ukaguzi wa Nyama.<br>Halmashauri inatarajia kukusanya kiasi cha Shs 21,650,000/= kutokana na ada ya ukaguzi wa nyama.<br>Machinjio<br>• Ng’ombe 2@5,000 x30 x 12 = 3,600,000/=<br>• Mbuzi 10@ 2,500x30x12 = 9,000,000/=</td><td>21,650,000.00</td></tr>
</table>

| KASMA | MAELEZO | MAKISIO 2021/2022 |
|---|---|---|
| | • Nguruwe 10@2,500 x30x12 = 9,00,000/=<br><br>**21,600,000/=**<br><br>**Leseni za uvuvi wa samaki/Kibali cha kusafirisha Samaki.**<br>• Wavuvi 5@10,000 = sh 50,000/= | |
| 120110 | **Ada ya usajili wa vikundi**<br><br>Halmashauri inatarajia kukusanya ada za usajili wa vikundi vipya 40@ 20,000 Jumla sh. **800,000.00** | **800,000.00** |
| | **Ada ya Upimaji Mashamba**<br><br>Halmashauri inatarajia kukusanya **sh**. **3,120,000.00** ikiwa ni ada ya upimaji mashamba. (Vijiji 12 x watu 4 x 65,000/=) | **3,120,000.00** |
| | **Umilikishwaji wa Ardhi /viwanja**<br><br>Halmashauri inategemea kukusanya Sh 30,000,000 ada ya umilikishaji wa ardhi. (Viwanja 600 x 50,000/= 30,000,000/=) | **30,000,000.00** |
| | Vibali vya Ujenzi<br><br>Halmashauri inategemea kukusanya Sh 1,500,000 ya vibali vya ujenzi. (vibali 50x 30,000) | **1,500,000.00** |
| | Ada ya Pango za ukodishaji wa mali za Halamashauri shilingi **23,160,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:-<br><br>• Nyumba za kuishi<br>➢ (Nyumba 4 x150,000= 600,000 x12) = 7,200,000/=<br>➢ (Nyumba 4 x100,000= 400,000x12) = 4,800,000/=<br>➢ (Nyumba 1 x80,000= 80,000 x 12) = 960,000/=<br>➢ (Nyumba 1 x200,000= 200,000 x12) = 2,400,000/=<br>• Ukumbi wa Halmashauri (200,000@tukio) x 12= 2,400,000<br>• Vyumba vya Ofisi 7 (450,000x12= 5,400,000) | **23,160,000.00** |
| | **Stendi ya Mabasi Ndanda**<br><br>Halmashauri inatarajia kukusanya S**h 44,244,000./=** kutoka katika stendi | **44,244,000.00** |

| KASMA | MAELEZO | MAKISIO 2021/2022 |
|---|---|---|
| | ya mabasi Ndanda wastani wa shs. 3,687,000/=kwa mwezi<br>• Mabasi makubwa 27 x siku 30 x2,000 x12 = shs.19,440,000/=<br>• Mabasi madogo (Coster) 54 x30 x 1,000 x 12 = shs 19,440,000/=<br>• Mabasi madogo (HIACE) 13 x30 x 1,000 x 12 = shs 4,680,000/=<br>• Pikipiki/ Bajaji 3 x siku 30 x 300 x 12 = shs 324,000/=<br>• Choo 1,000 x siku 30 x 12 = shs 360,000/= | |
| | **A.JUMLA YA MAPATO HALISI (PROPER OWN SOURCE)** | **2,285,766,000.00** |

**B. Jedwali Na.5: Kuonesha Mtiririko wa Mapato toka vyanzo Lindwa**

| KASMA | MAELEZO | MAKISIO 2021/2022 |
|---|---|---|
| 20106 | **CHF**<br>Halmashauri inakadiria kukusanya shilingi **15,000,000/=** kutoka kwenye kaya 500 kwa shilingi 30,000 kwa kaya kwa mwaka wa fedha 2021/2022. | **15,000,000.00** |
| 20106 | **USER FEES**<br>Halmashauri inakadiria kukusanya shilingi **100,494,522/=** kutoka kwenye Vituo 37 vya kutolea huduma za Afya kwa mwaka wa fedha 2021/2022 | **100,495,000.00** |
| 120105 | **NHIF**<br>Kiasi cha **Tshs. 35,000,000.00** kinatarajiwa kukusanywa kutoka mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya | **35,000,000.00** |
| 20106 | **DRUG REVOLVING FUND ( MFUKO WA DAWA)**<br>Halmashauri inakadiria kukusanya shilingi **20,000,000.00** kutoka katika duka la dawa la Halmashauri | **20,000,000.00** |
| 120103 | **Ada ya shule za Sekondari (A'Level)**<br>Halmashauri inatarajia kukusanya **Sh. 134,960.,000.00** ikiwa ni ada ya shule za sekondari (A'Level) kutoka<br>• Ndanda Sekondari. Wanafunzi 916 x 70,000 = 64,120,000.00<br>• Chidya Sekondari Wanafunzi 443 x 70,000 = 31,010,000.00<br>• Ndwika Sekondari Wanafunzi 415 x 70,000 = 29,050,000.00 | **134,960,000.00** |

<table>
<tr><td></td><td>• Chiungutwa Sekondari Wanafunzi 154 x 70,000 = 10,780,000.00</td><td></td></tr>
<tr><td>110815</td><td>Mfuko wa Elimu<br>Halmashauri inakisia kukusanya shilingi 630,000,000.00 kutokana na Ushuru wa mazao (Mfuko wa Elimu) kwa mchanganuo ufuatao:-
<table>
<tr><th>Zao</th><th>Tani Tegemewa (2021/22)</th><th>Bei kwa kilo</th><th>Ushuru kwa kilo</th><th>Kiasi tegemewa</th></tr>
<tr><td>Korosho</td><td>26,000</td><td>2,000</td><td>20.00</td><td>520,000,000.00</td></tr>
<tr><td>Ufuta</td><td>5,500</td><td>2,000</td><td>20.00</td><td>110,000,000.00</td></tr>
<tr><td colspan="4">JUMLA</td><td>630,000,000.00</td></tr>
</table></td><td>630,000,000.00</td></tr>
<tr><td>120103</td><td>Fedha za Elimu ya Kujitegemea<br>1. Shule za Msingi Sh. 109,000,000.00<br>2. Shule za Sekondari Sh.208,452,000.00</td><td>317,452,000.00</td></tr>
<tr><td></td><td>B. JUMLA YA MAPATO LINDWA (PROTECTED SOURCES)</td><td>1,252,907,000.00</td></tr>
<tr><td></td><td>JUMLA KUU (A&B)</td><td>3,538,673,000.00</td></tr>
</table>

**Jedwali Na. 6: Muhtasari wa Makadirio ya Mapato Kutokana na Mafungu mbalimbali.**

| **Fungu/Maelezo** | **Makadirio 2021/22** |
|---|---:|
| Vyanzo vya Halmashauri | 3,538,673,000.00 |
| **JUMLA** | **3,538,673,000.00** |
| **Vyanzo vingine:** | |
| Ruzuku – Mishahara | 27,696,792,000.00 |
| Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC) (Nyuki 4m, M/Jamii 12m, Biashara 11m, Ukaguzi Ndani 16m, Ardhi+Maliasili 8m, Mipango 46,203,000 na Mazingira 12m, Afya 75,225,000 ,Elimu Msingi 480,994,000, Elimu Sekondari 336,691,000, Kilimo 11,058,600, Mifugo 7,372,400, Ujenzi 18,473,000 na Sheria 5m, | 1,182,639,000.00 |
| Ruzuku ya Fidia (GPG-Utawala) | 80,232,000.00 |
| Miradi ya Maendeleo | 11,898,954,000.00 |
| **JUMLA NDOGO** | **40,858,617,000.00** |
| **JUMLA KUU** | **44,397,290,000.00** |

**Jedwali Na. 7: Mlinganisho wa Mategemeo ya Miradi ya Maendeleo 2020/21 & 2021/22**

| S/N | JINA LA MRADI | 2020/2021 | 2021/2022 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mfuko wa Jimbo (CDF) | 78,664,000.00 | 78,664,000.00 |
| 2 | Ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri | 1,000,000,000.00 | 1,000,000,000.00 |
| 3 | Ujenzi wa Ofisi za Halmashauri | 1,000,000,000.00 | 1,000,000,000.00 |
| 4 | Umaliziaji wa vyumba vya Madarasa S/M | 225,034,000.00 | 0.00 |
| 5 | Elimu bila malipo - Msingi | 900,381,000.00 | 939,438,000.00 |
| 6 | Elimu bila malipo - Sekondari | 1,379,800,000.00 | 1,672,020,000.00 |
| 7 | Umaliziaji wa Zahanati | 200,000,000.00 | 200,000,000.00 |
| 8 | Umaliziaji wa Maabara | 390,000,000.00 | 390,000,000.00 |
| 9 | UNICEF | 10,000,000.00 | 10,000,000.00 |
| 10 | Mfuko wa Afya wa Pamoja (HSBF) | 513,751,000.00 | 513,751,000.00 |
| 11 | Mpango wa EP4R | 400,000,000.00 | 400,000,000.00 |
| 12 | TASAF | 5,173,282,000.00 | 5,173,282,000.00 |
| 13 | Uboreshaji wa Vituo vya Afya (RBF) | 323,798,000.00 | 0.00 |
| 14 | SWASH | 509,800,000.00 | 509,800,000.00 |
| 15 | Mpango wa Lishe Bora | 11,999,000.00 | 11,999,000.00 |
| **JUMLA MIRADI YA MAENDELEO** | | **12,116,509,000** | **11,898,954,000.00** |

Mhe. Mwenyekiti, makadirio ya mwaka 2021/2022 ni jumla ya shilingi **44,397,290,000.00** ukilinganisha na mwaka 2020/2021 shilingi **34,639,132,000.00** Makadirio haya yamepanda kwa asilimia **28.17** ya makadirio ya mwaka 2020/2021. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa fedha za Mishahara ya ajira mpya, fedha za Mitihani, na fedha za elimu bila malipo kulikotokana na ongezeko la wanafunzi.

.

## F: MAKISIO YA MATUMIZI 2021/2022

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri inakadiria kutumia jumla shilingi **44,397,290,000** kwa mchanganuo ufuatao:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| i) | Mishahara | Sh. | 27,696,792,000.00 |
| ii) | Matumizi mengineyo | Sh. | 1,262,871,000.00 |
| iii) | Miradi ya Maendeleo | Sh. | 11,898,954,000.00 |
| iv) | Mapato ya ndani ya Halmashauri | Sh. | 3,538,673,000.00 |
| | **JUMLA KUU BAJETI** | **Sh.** | **44,397,290,000.00** |

**MAKISIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2021/2022 KAMATI MBALIMBALI KAMA IFUATAVYO:**

| S/N | KAMATI | OC - SERIKALI KUU | OC - MAPATO YA NDANI | MISHAHARA | MIRADI | | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | MAPATO YA NDANI | NDANI (SERIKALI KUU) | NJE (WAHISANI) | |
| 1 | Elimu, Afya na Maji | 1,107,764,000 | 512,957,000 | 22,600,480,000 | 880,000,000 | 4,201,458,000 | 1,445,550,000 | **30,748,209,000** |
| 2 | Ujenzi, Uchumi na Mazingira | 76,904,000 | 119,000,000 | 2,026,458,000 | 495,755,400 | 0 | 5,173,282,000 | **7,891,399,400** |
| 3 | Fedha Utawala Mipango | 78,203,000 | 1,338,409,600 | 3,069,854,000 | 168,551,000 | 1,078,664,000 | 0 | **5,733,681,600** |
| 4 | Kuthibiti Ukimwi | 0 | 24,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | **24,000,000** |
| **JUMLA KUU** | | **1,262,871,000** | **1,994,366,600** | **27,696,792,000** | **1,544,306,400** | **5,280,122,000** | **6,618,832,000** | **44,397,290,000** |

**NB:** Fedha za mapato ya ndani zitakazotumika kwenye miradi ya Maendeleo 40% ya makusanyo yasiyolindwa kwa kamati mbalimbali:-

- Kamati ya Elimu, Afya na Maji shilingi **880,000,000**
- Kamati ya Ujenzi, Uchumi na Mazingira shilingi **495,755,400**
- Kamati Fedha, Utawala na Mipango shilingi **168,551,000**

## H: CHANGAMOTO:

Mhe; Mwenyekiti, pamoja na rasimu hii Halmashauri imepata changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya 2020/2021

1. Upungufu wa Watumishi katika Idara Mbalimbali
2. Kuchelewa kupokea fedha za Miradi ya Maendeleo
3. Ukosefu wa Ofisi za Kudumu hii baada ya Halmashauri yetu kuhamia katika eneo lake la Utawala.
4. Ukosefu wa Nyumba za Watumishi
5. Kuchelewa kwa malipo mbalimbali kunakosababishwa na kuchelewa kupata vifungu vya malipo kutoka OR – TAMISEMI kwa fedha zilizopokelewa nje ya bajeti.
6. Upungufu wa magari, ikiwemo gari la Wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya

**I: UFUMBUZI:**

Ufumbuzi wa Changamoto hizo ni pamoja na:-

1. Katika Bajeti ya mwaka 2021/22 Halmashauri imeomba kibali cha kuajiri Watumishi **1,492**.
2. Halmashauri itaendelea kuwasiliana na OR – TAMISEMI kukumbushia fedha za miradi, pamoja na kutumia fedha za mapato ya Ndani kutekeleza baadhi ya miradi.
3. Halmashauri imetuma barua OR – TAMISEMI kuomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi Mpya.
4. Halmashauri itaendelea kuwasiliana na OR – TAMISEMI kukumbushia maombi ya fedha kwa ajili ya maombi ya ujenzi wa nyumba za Watumishi.
5. Halmashauri itaendelea kuwasiliana na OR – TAMISEMI na pia kutuma maafisa wake pindi tatizo la kuchelewa malipo inapojitokeza.
6. Katika bajeti ya mwaka 2021/21 Halmashauri imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari, pia itaendelea kufuatilia ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kutupatia gari la Wagonjwa katika kituo cha Afya Chiwale.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **44,397,290,000.00** kati ya fedha hizo, shilingi **27,696,792,000.00** ni kwa ajili ya mishahara, shilingi **3,257,237,600** ni matumizi ya kawaida kwa ajili ya kuendesha ofisi na shilingi **13,443,260,400** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mhe; Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.



Changwa M. Mkwazu,
MKURUGENZI MTENDAJI (W),
MASASI.

## KIAMBATISHO CHA MCHANGANUO WA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI YA HALMASHAURI YA WILAYA (2021/2022-2023/2024)

### I. MISHAHARA:

Kwa mwaka wa fedha **2021/22** kiasi cha shilingi **27,696,792,000.00** kimeombwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya yetu na kitatumika kwa mchanganuo wa kiidara kama ifuatavyo:-

| S/N | KIFUNGU | IDARA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 1 | 5004 | Mshahara GSs and Above | 2,122,562,000 |
| 2 | 5006 | Utawala na Elimu Watu wazima | 209,424,000 |
| 3 | 5007 | Elimu Msingi | 14,166,216,000 |
| 4 | 5008 | Elimu Sekondari | 5,775,396,000 |
| 5 | 5010 | Huduma za Afya | 531,417,000 |
| 6 | 5011 | Huduma – Kinga | 236,292,000 |
| 7 | 5012 | Vituo vya Afya | 1,026,928,000 |
| 8 | 5013 | Zahanati | 586,212,000 |
| 9 | 5014 | Ujenzi | 89,166,000 |
| 10 | 5017 | Maji Vijijini | 68,595,000 |
| 11 | 5031 | Mishahara ya Watendaji wa Vijiji (VEOs) | 947,292,000 |
| 12 | 5033 | Kilimo | 873,180,000 |
| 13 | 5034 | Mifugo | 1,064,112,000 |
| | | **JUMLA KUU MSHAHARA** | **27,696,792,000** |

## II. MAKISIO YA MATUMIZI YA MAPATO YA NDANI II:

Jumla ya shilingi **3,538,673,000.00** zinategemewa kukusanywa na kugawanywa katika Sekta mbalimbali za Halmashauri kwa mwaka fedha **2021/2022** ili kutekeleza shughuli mbalimbali za Kiutawala na Miradi mbalimbali ya Halmashauri kama ifuatavyo:-

| S/N | KASMA | IDARA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 1 | 500A | Utawala | 255,574,400.00 |
| 2 | 503A | Sera, Mipango & Usimamizi | 40,000,000.00 |
| 3 | 514A | Sheria | 10,000,000.00 |
| | | Ujenzi | 8,000,000.00 |
| 4 | 500A | Uchaguzi | 8,000,000.00 |
| 5 | 515A | Ukaguzi wa Ndani | 15,000,000.00 |
| 6 | 500B | Mishahara | 160,000,000.00 |
| 7 | 500B | Utumishi | 168,127,200.00 |
| 8 | 500C | Madiwani | 437,854,000.00 |
| 9 | 502A | Fedha Utawala | 12,000,000.00 |
| 10 | 502B | Fedha Final Accounts | 16,000,000.00 |
| 11 | 502C | Fedha Matumizi | 15,000,000.00 |
| 12 | 502D | Fedha Mapato | 20,000,000.00 |
| 13 | 516A | Ugavi | 10,000,000.00 |
| 14 | 502E | Biashara na Uchumi | 10,000,000.00 |
| 15 | 506D | Ushirika na Masoko | 10,000,000.00 |
| 16 | 507D | Elimu (M) Utamaduni | 10,000,000.00 |
| 17 | 508A | Afya (Watoto chini ya Miaka 5) LISHE | 40,904,000.00 |
| 18 | 512A | Ardhi Utawala | 30,000,000.00 |
| 19 | 512G | Maliasili Uwindaji | 8,000,000.00 |
| 20 | 512F | Maliasili Utawala | 8,000,000.00 |
| 21 | 519A | Maliasili Nyuki | 8,000,000.00 |
| 22 | 518A | Habari na Mawasiliano | 10,000,000.00 |
| 23 | 527A | Maendeleo ya Jamii | 15,000,000.00 |
| 24 | 527B | UKIMWI | 24,000,000.00 |
| 25 | 501A | Mazingira | 10,000,000.00 |
| 26 | | Mifugo na Uvuvi | 12,000,000.00 |
| | | **60% Mapato ya Ndani (Matumizi Mengineyo)** | **1,371,459,600.00** |
| | | **MIRADI YA MAENDELEO** | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 27 | 527B | Mchango wa Wanawake, Vijana na Walemavu (10%) | 228,576,600.00 |
| 28 | 506B | Miradi ya Maendeleo – KILIMO, MIFUGO NA UVUVI (40% ya Produce cess) | 267,178,800.00 |
| 29 | 508A | Kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Afya Chiungutwa | 50,000,000.00 |
| 30 | 508A | Ujenzi wa Kituo cha Afya Namatutwe | 200,000,000.00 |
| 31 | 503B | Ununuzi wa Gari (Land Cruiser Hard top) | 125,000,000.00 |
| 32 | 500A | Ununuzi wa Pikipiki 16 za Watendaji wa Kata | 36,800,000.00 |
| 33 | 503A | Usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo | 6,751,000.00 |
| | | **40% Mapato ya Ndani -Miradi ya Maendeleo** | **914,306,400.00** |
| | | **VYANZO LINDWA** | |
| 34 | 508A | CHF | 15,000,000.00 |
| 35 | 508A | USER FEE | 100,495,000.00 |
| 36 | 508A | NHIF | 35,000,000.00 |
| 36 | 508A | DRUGS REVOLVING FUND (DRF) | 20,000,000.00 |
| 38 | 509A | ADA YA SEKONDARI | 134,960,000.00 |
| 39 | | **MFUKO WA ELIMU** | 0.00 |
| | 506B | A. ELIMU MSINGI - 387,900,000 | 630,000,000.00 |
| | 509A | B. ELIMU SEKONDARI – 242,100,000 | |
| 40 | | **FEDHA ZA ELIMU YA KUJITEGEMEA** | 0.00 |
| | | A. ELIMU MSINGI | 109,000,000.00 |
| | | B. ELIMU SEKONDARI | 208,452,000.00 |
| | | **Jumla Ndogo-Mapato Lindwa** | **1,252,907,000.00** |
| | | **JUMLA MATUMIZI MAPATO YA NDANI** | **3,538,673,000.00** |

### III. MATUMIZI MENGINEYO (OC):

Kwa mwaka wa fedha **2021/22** Halmashauri yetu inaomba jumla ya shilingi **1,262,871,000.00** ili kugharamia matumizi mengineyo ya kiidara kama inavyoonesha katika mchanganuo ufuatao:-

| S/N | KIFUNGU | IDARA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 1 | 500A | Utawala | 32,206,000.00 |
| 2 | 500B | Utumishi | 16,046,400.00 |
| 3 | 500C | Madiwani | 31,974,500.00 |
| 4 | 503E | Biashara na Uchumi | 11,000,000.00 |
| 5 | 514A | Sheria | 5,000,000.00 |
| 6 | 505A | Ukaguzi wa Ndani | 16,000,000.00 |
| 7 | 503B | Mipango | 46,203,000.00 |
| 8 | 507B | Elimu Msingi | 570,833,100.00 |
| 9 | 509B | Elimu Sekonari | 385,479,000.00 |
| 10 | 512A | Ardhi Utawala | 4,000,000.00 |
| 11 | 508A | Afya | 48,622,000.00 |
| 12 | 508A | Afya- On call allowances | 26,603,000.00 |
| 13 | 511A | Ujenzi | 18,473,000.00 |
| 14 | 519B | Maliasili Nyuki | 4,000,000.00 |
| 15 | 516A | Maliasili Utawala | 4,000,000.00 |
| 16 | 527A | Maendeleo ya Jamii | 12,000,000.00 |
| 17 | 506A | Kilimo + Mifugo ( Kilimo 11,058,600 na Mifugo 7,372,400) | 18,431,000.00 |
| 18 | 501A | Mazingira | 12,000,000.00 |
| | **JUMLA MATUMIZI MENGINEYO (OC)** | | **1,262,871,000.00** |